TANGAZO LA SERIKALI Na. 581 la tarehe 12/7/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 605 la 2019

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada Na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada Na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka 2019, ambayo katika marekebisho haya itarejewa kama Sheria Ndogo Kuu.

Marekebisho ya kanuni ya 2

2. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kanuni ya 2 kwa kuongeza katika mpangalio wake wa kialufabeti tafsiri ya msamiati-

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;".

Marekebisho ya kanuni ya 7

3. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kanuni ya 7, kwa-

(a) kuunda maudhui ya kanuni ya 7 kama maudhui kanuni ndogo ya 7 (1); na
(b) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (1) kama ilivyoundwa hapo juu yafuatayo:

"(2) Mtu yeyote au kampuni itakayohitaji kusafirisha-

(a) mazao au bidhaa zitokanazo na mazao

yanayozalishwa ndani ya Halmashauri; au

(b) madini ya ujenzi,

(c) baada ya muda uliotajwa katika kanuni ndogo ya 7(1) ya Sheria Ndogo hii atatakiwa kuwa na kibali maalumu cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa.".

Marekebisho ya kanuni ya 12

4. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika kanuni ya 12 (1), kwa kufuta aya (c) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(c) atasafirisha mazao au bidhaa itokanayo na mazao yanayozalishwa ndani ya Halmashauri au madini ya ujenzi nje ya muda unaoruhusiwa chini ya Sheria Ndogo hii bila kibali maalumu cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa.".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

5. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho katika Jedwali la kwanza kwa-

(a) kufuta Sehemu ya Kwanza ya Jedwali hilo na kuiandika upya kama ifuatavyo:

SEHEMU YA KWANZA
USHURU WA HUDUMA YA MACHINJIO

| Namba | mnyama | kiasi kwa siku | idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | ng'ombe | 3,000 | 1 |
| 2 | nguruwe | 2,000 | 1 |
| 3 | mbuzi/kondoo | 1,500 | 1 |

(b) kufuta Sehemu ya Tatu ya Jedwali hilo na kuiandika upya kama ifuatavyo:

SEHEMU YA TATU
USHURU WA VIBANDA

| Namba | Kibanda | Kiasi cha Ushuru | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Soko kuu Mwanga, TANESCO na Uwanja wa CD Muya | 20,000 | kwa mwezi |
| 2 | Soko la Old Mwanga | 20,000 | kwa mwezi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Stendi Kuu ya Mabasi | 20,000 | kwa mwezi |
| 4 | Soko la Mgagao | 10,000 | kwa mwezi |

(c) kufuta Sehumu ya Saba ya Jedwali hilo na kuiandika upya kama ifuatavyo:

SEHEMU YA SABA
USHURU WA MAEGESHO NDANI YA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya chombo cha usafiri | Kiasi | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Malori | 3,000 | kwa siku |
| 2 | Magari madogo ya watu binafsi yasiyo ya biashara | 500 | kwa siku |
| 3. | Mabasi na costa za kusafirisha abiria na magari mengine madogo ya biashara | 1,000 | kwa siku |

(d) kufuta Sehumu ya Kumi na Tatu ya Jedwali hilo na kuiandika upya kama ifuatavyo:

SEHEMU YA KUMI NA TATU
A: USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba | Aina ya Madini | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Kwa kila Mita moja ya ujazo | |
| | (i) mchanga | 3,000/= kwa kila safari |
| | (ii) mawe | 2,500/= kwa kila safari |
| | (iii) Jipsum | 2,000/= kwa kila safari |
| | Tofari za sementi za | |
| | (i) inchi sita | 50 |
| | (ii) inchi tano | 50 |
| | (iii) tofari za kuchoma | 10 |

B: MADINI MENGINEYO

| Namba | Aina ya Madini | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Madini mengineyo yasiyokuwa madini ya ujenzi, madini ya kutengeneza vito na mapambo na vifaa mbalimbali | Asilimia tatu ya bei ya soko (1.5%) |

(e) kuongeza Sehemu zifuatazo mara baada ya Sehumu ya Kumi na Nane ya Jedwali hilo:

SEHEMU YA KUMI NA TISA
ADA YA MAZAO YA MALI ASILI

| Namba | Aina ya Mazao | Kiasi cha Mzao | kisi cha Ushuru |
|---|---|---|---|
| 1 | Mkaa | Gunia moja | 1,000/= |
| 2. | mbao | 2x2<br>2x4 | 200/= |
| | | 2x6<br>2x8 | 300/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Mirunda | Kipande | 300/= |
| 4. | Nguzo | Kipande | 1,000/= |
| 5. | Ukindu | Bello | 1,000/= |
| 6. | Fito | kipande | 50/= |
| 7. | Magogo | | |
| | (i) Ada ya Magogo Viwandani kwa kila mita moja ya mraba | 15,000/= | |
| | (ii) ushuru wa magogo kwa toyo | 15,000/= | |
| | (iii) ushuru wa magogo kwa Pick up | 50,000/= | |
| | (iv) ushuru wa magogo kwa canter | 120,000/= | |
| | (v) ushuru wa magogo kwa fuso | 180,000/= | |
| | (vi) Ada ya Gogo moja | 1,000/= | |
| 8. | Asali | kila lita moja | 500/= |

## SEHEMU YA ISHIRINI
## ADA YA KIBALI CHA KUONYESHA MPIRA, GYM NA SHUGHULI ZA UTALII

| Namba | Aina | kiasi | muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Kibali cha kuonyesha mpira kwenye vibanda | 100,000/= | kwa mwaka |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Kibali ch akuendesha shughuli za GYM | 100,000/= | kwa mwaka |
| 3. | Kibali cha shughuli za Utalii | Watoto chini ya miaka 18 Tsh. 2,00 | Kwa siku |
| | Kibali cha kutembelea eneo la kitalii kwa mtu mmoja | Raia wa kigeni Tsh. 20,000 | Kwa siku |
| | | Watanzania Tsh. 5,000 | Kwa siku |
| | | 20,000/= | kwa siku. |
| | Kibali cha gari kufika katika eneo la Kitalii | 20,000/= | Kwa siku |
| | Kibali kwa mtu binafsi au Kampuni kuendesha shughuli za Kitalii | 100,000/= | kwa mwaka |
| | Kibali cha sherehe | 30,000/= | Kwa siku |

SEHEMU YA ISHIRINI NA MOJA
USHURU WA SOKO NA MAGULIO SIKU YA MAGULIO

| Namba | sehemu | ushuru | muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Soko kuu Mwanga | 500 | Kwa siku ya soko/gulio |
| 2 | Masoko/magulio yaliyopo nje ya mamlaka ya mji mdogo Mwanga | 500 | Kwa siku ya soko/gulio |

SEHEMU YA ISHIRINI NA MBILI
ADA YA UZOAJI TAKA NA TAKA NGUMU

| Namba | Aina ya Jengo/ Biashara | Ushuru | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Hoteli | 10,000 | Mwezi |
| 2 | Makazi | 2,000 | Mwezi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Baa | 5,000 | Mwezi |
| 4 | Maduka | 3,000 | Mwezi |
| 5 | Nyumba za kulala wageni | 5,000 | Mwezi |
| 6 | Mghahawa | 5,000 | Mwezi |
| 7. | Gereji na uchomeleaji | 3,000 | Mwezi |
| 8. | Saluni | 3,000 | Mwezi |
| 9 | Mashine ya kusaga | 3,000 | Mwezi |

SEHEMU YA ISHIRINI NA TATU
ADA YA LESENI YA UVUVI

| **Namba** | **Aina ya leseni** | **Ada ya leseni kwa mwaka** |
|---|---|---|
| 1. | Leseni ya Biashara ya Samaki | 23,000/= |
| 2 | Leseni ya Uvuvi | 23,000/= |
| 3 | Leseni ya chombo cha uvuvi | 23,000/= |
| | | |

SEHEMU YA ISHIRINI NA NNE
ADA YA USHURU WA MAZAO YA SAMAKI

| Namba | kipimo | aina samaki | kiwango cha ushuru |
|---|---|---|---|
| 4. | Ndoo ya Lita 20 (Wakavu au wabichi) | Perege, Kambale | 2,000 kwa ndoo |

SEHEMU YA ISHIRINI NA TANO
ADA YA UKAGUZI NA VIBALI VYA UJENZI

| **Namba** | **Aina ya jengo** | **Ada ya ukaguzi** | **Ada ya kibali** |
|---|---|---|---|
| 1 | Ghorofa 1 | 50,000 | 100, 000/= |
| 2 | Ghorofa 2 Na Kuendelea | 50,000 | 150, 000/= |

*Tangazo la Serikali Na.581 (Linaendelea.)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Nyumba Za Biashara | 30,000 | 100,000/ |
| 4 | Ghala Au Bohari | 50,000 | 100, 000/= |
| 5 | Kituo cha Mafuta | 50,000 | 200, 000/= |
| 6 | Nyumba Za Makazi | 20,000 | 30, 000/= |
| 7 | Nyumba Za Makazi Na Biashara | 30,000 | 50, 000/= |
| 8 | MAJENGO MENGINE<br>i. Jengo Kubwa<br>ii. Jengo Dogo | 100,00<br>20,000 | 200,000<br>30,000 |
| **9** | Uzio Wa Seng'enge | 10,000 | 25,000/= |
| 10 | Uzio Wa Ukuta | 20,000 | 40,000/= |
| 11 | Minara ya Mawasiliano | 200,000 | 300,000 |
| 12 | Marekesho Yeyote Ya Jengo | 10,000 | 30,000/= |
| 13. | Majengo ya shule/taasisi | 50,000 | 200,000 |

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ulioitishwa na kufanyika tarehe 1/3/2023 na muhuri wa Halmashauri ilibandikwa mbele ya:-

MWAJUMA A. NASOMBE,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

MHE. Dr. SALEHE R. MKWIZU,
Mwenyekiti,
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
WAZIRI wa NCHI OR-TAMISEMI,